



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HB/W:20/1 Vol/357

06/10/2023

TANGAZO KWA WATUMISHI WOTE

Serikali kupitia sera yake ya kuboresha maisha ya watumishi wake imeamua kutoa mikopo kwa watumishi wa Serikali za Mitaa kwa ajili ya ununuzi wa magari, samani, pikipiki na matengenezo ya vyombo vya usafiri. Serikali imetoa Tshs. 350,000,000/=.

Watumishi wote mnakaribishwa kutuma maombi kwa ajili ya mkopo tajwa hapo juu kwa masharti yafuatayo:

- Mkopo utatolewa kwa mtumishi mwenye Ajira ya Masharti ya Kudumu.
- Mkopo utatolewa kwa Mtumishi aliyethibitishwa kazini.
- Mkopaji anatakiwa kubakiwa na 1/3 ya mshahara wake baada ya makato ambayo yatareješhwa kwa kipindi kisichozidi miezi 72 (miaka 6)
- Mikopo hii hainunui deni kutoka taasisi nyingine za fedha na hakuna kuongeza mkopo hadi uishe
- Mkopaji atalipa "service charge" 3% na "Protect fund" 1% kutoka kwenye mkopo atakaokopa
- Mkopo unaotolewa kwa mtumishi hauna riba
- Mkopo utatolewa kwa mtumishi mwenye mwenendo mzuri kazini na utendaji mzuri wa kazi katika Utumishi wa Umma na ambaye hana mashauri ya kinidhamu.
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 16/10/2023 saa 9:30 mchana

Maelekezo ya kufuata kwa mkopaji.

Mkopo huu utaombwa kwa njia ya mtandao (*internet*) kwa kufuata njia zifuatazo:-


- Ingiza link ya kuomba mkopo ambayo ni als.muse.go.tz
- Nenda sehemu ya *Register* ambapo utaingiza taarifa zako zote za Kiutumishi kama zinavyosomeka kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS).
- Nenda sehemu ya *Verify Details* ambapo utatumiwa *Password* kwenye email yako binafsi
- Nenda sehemu ya *username* ambapo utaweka *check number* yako na utaweka *password* yako kama ulivyotumiwa kwenye email yako.

- Ukishaingiza *password* uta *login* ambapo utapewa nafasi ya kubadili *password* au kuendelea na *password* uliyotumiwa.
- Utafungua mfumo na kuingia sehemu ya *Advance Loan*.
- Utakwenda moja kwa moja hadi sehemu ya *Apply Loan*.
- Utajaza taarifa zako za mkopo na mwisho utakwenda sehemu ya *Submit*.
- Baada ya hapo utasubiri maelekezo mengine kutoka kwa mwajiri kama utakuwa umekidhi sifa na utakuwa umepitishwa na Kamati ya Mikopo ya Halmashauri.
- Kwa usaidizi zaidi mwombaji atawasiliana na Bw. Pereus R. Kyaruzi kwa namba 0758326318/0717709106.

NB:- Taarifa za mwombaji ambaye zitatofautiana na zilizo kwenye Mfumo wa HCMIS basi mtumishi huyo hatopata huduma ya kuomba mkopo wa Serikali kwa kuwa hatoweza kujisajili.

VIWANGO VYA MIKOPO.

Aina ya Mkopo	Ngazi ya Mshahara	Kiwango cha juu cha mkopo	Muda wa Marejesho
Mkopo Taslimu kwa ajili ya Ununuzi wa magari, pikipiki, samani na matengenezo ya vyombo vya usafiri	TGS A-C TGTS A-C TGHS A-C TGOS A-C TGHOS A-C	Milioni 15,000,000/=	Miezi 72 (Miaka 6)
	TGS D-F TGTS D-F TGHS D-F	Milioni 30,000,000/=	Miezi 72 (Miaka 6)
	TGS G-H TGTS G-H TGHS G-H	Milioni 40,000,000/=	Miezi 72 (Miaka 6)
	LSSE 1-4 TGTS I TGHS I-J	Milioni 50,000,000/=	Miezi 72 (Miaka 6)


 Changwa M. Mkwazu
 Mkurugenzi Mtendaji (W)
BUNDA.

MKURUGENZI MTENDAJI (W) BUNDA
HALMASHAURI YA WILAYA BUNDA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), S.L.P 126, Bunda-Mara, Simu: Namba 028 2621055, Fax Namba: 0282621264, tovuti: www.bundadc.go.tz, Barua Pepe: ded@bundadc.go.tz